HOTUBA YA MHESHIMIWA MIZENGO P. PINDA (MB.) WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA KILELE CHA MAONESHO YA MIAKA 50 YA MUUNGANO VIWANJA VYA MNAZI MMOJA, DAR ES SALAAM, TAREHE 19 APRILI 2014

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Makamu wa Rais;

Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed; Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar;

Mheshimiwa Said Meck Sadiki; Mkuu wa Mkoa wa
Dar es Salaam;

Balozi Ombeni Sefue; Katibu Mkuu Kiongozi wa
Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kuwepo hapa siku ya leo ili kuhitimisha **maonesho ya kuadhimisha Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**.

Pili, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waandaaji wa hafla hii kwa kunialika kuhitimisha maonesho haya ya siku tano (5) ambayo ni ya kipekee katika historia ya Muungano wetu yaliyofunguliwa na Mheshimiwa Seif Sharif Hamadi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Napenda pia kuipongeza Kamati ya Kitaifa, iliyoandaa maonesho haya ambayo kwa hakika yamefana sana. Aidha, niwashukuru Wananchi wote mliojitokeza kwa wingi kushiriki katika maonesho haya. Ni imani yangu kuwa mmeelimika na kujifunza mengi kuhusu historia ya Muungano wetu kupitia maonesho haya.

Historia ya Muungano

Ndugu Wananchi,

Historia ya Muungano inaonyesha kwamba mengi yamefanyika katika kipindi cha miaka 50 ya Muungano tangu Waasisi wa Muungano huu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika wakati huo na Hayati Abeid Amani Karume, Rais wa Zanzibar, kukubali kuanzisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunu tuliyonayo katika kipindi hiki ni umoja wetu, amani na utulivu tulionao. Tumeishi kwa pamoja kama ndugu, tumekuwa na amani na tumeishi kwa utulivu katika miaka yote 50 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni fahari yetu sisi sote kama Watanzania tunapoadhimisha Miaka 50 ya Muungano wetu tukiwa na umoja wa Kitaifa uliojengeka katika misingi ya Amani, Mshikamano na Utulivu.

Maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano

Ndugu Wananchi;

Kama mtakumbuka, sherehe za maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano, zilizinduliwa rasmi tarehe 1 Machi 2014, kule Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Maonesho haya yalishirikisha Wizara na Taasisi za Muungano kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Ni imani yangu kuwa Wananchi wamepata fursa ya kujionea wenyewe ushirikiano uliopo kwa Watanzania wote na katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Wito wangu kwenu ni kuomba ushirikiano huu uendelezwe sasa na vizazi vijavyo.

Ndugu Wananchi;

Lengo la kuwa na maonesho haya ni kutangaza mafanikio tuliyoyapata tokea kuasisiwa kwa Muungano wetu mwaka 1964. Kwa kutumia maonesho haya Wananchi wamepata fursa ya kupata elimu ya masuala ya Muungano, namna yanavyotekelezwa pamoja na changamoto zilizopo na namna zilivyotatuliwa. Ninaamini kuwa, Wananchi wamejifunza mengi kupitia maonesho haya na wamepata fursa ya kipekee ya kutoa maoni ya kuimarisha Muungano wetu. Napenda kuwahakikishia Watanzania wote kuwa, maoni yaliyotolewa kuhusiana na Muungano yatafanyiwa kazi kwa umakini mkubwa, ili tuuenzi, tuulinde na kuudumisha Muungano wetu kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mafanikio ya Muungano

Ndugu Wananchi;

Tunayo kila sababu ya kujivunia Muungano wetu kwa kufikisha miaka 50 tokea kuasisiwa kwake. Ni dhahiri kuwa kuna mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya Nchi yetu katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Ni kweli pia kwamba Muungano wetu umeongeza mshikamano baina ya watanzania wote. Muungano wetu umeweka historia ya kipekee na umedumu kwa muda mrefu na kuweza kupata mafanikio ya aina yake barani Afrika. Ni Muungano wa pekee wa Nchi huru uliodumu baada ya jitihada za Nchi zingine kukwama.

Ndugu Wananchi;

Tangu maadhimisho haya yazinduliwe tarehe 1 Machi 2014, tumewasikia viongozi wetu kwa nyakati tofauti wakiongelea mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kipindi cha miaka 50. Mafanikio hayo ni mengi na yamekuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Ni jambo linalojidhihirisha kuwa Muungano huu ni nyenzo imara na muhimu katika kuimarisha umoja na udugu wetu. Watanzania wa pande zote mbili za Muungano wameungana katika misingi ya kiutamaduni na wanapata fursa ya kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hali hii imechangia katika kupunguza migawanyiko ya kijamii na kuondoa hisia za ukabila na ubaguzi miongoni mwao. Aidha, Muungano umeendelea kuwa utambulisho muhimu wa umoja wetu. Hivyo, hatuna budi kuadhimisha miaka 50 kwa kujivunia mafanikio hayo.

Changamoto za Muungano

Ndugu Wananchi;

Pamoja na mafanikio yenye kutia moyo yaliyopatikana katika kipindi hiki cha Miaka 50 ya Muungano, ni kweli kwamba bado Muungano wetu unakabiliwa na changamoto kadhaa kama ilivyo kwa Nchi nyingine mbalimbali duniani zilizoungana. Baadhi ya changamoto hizo ni za kiuchumi na kisiasa. Aidha kuna changamoto za kiutendaji, kisera na kisheria ambazo zimechangia kupunguza kasi ya maendeleo ya Wananchi katika baadhi ya Sekta muhimu. Katika kukabiliana na changamoto hizo wapo wenye mtazamo wa kuziona changamoto hizo kama fursa ya kuimarisha Muungano na wapo wenye mtazamo hasi wa kuudhoofisha Muungano wetu.

Ndugu Wananchi;

Vilevile, uelewa mdogo wa Wananchi kuhusu mambo ya Muungano pia ni changamoto. Hata hivyo, Serikali zetu mbili zimeweka kipaumbele katika kuhakikisha changamoto zilizopo kwenye Muungano wetu zinafanyiwa kazi ili kupata suluhisho lake hivyo kuongeza kasi ya maendeleo, utulivu na amani ya Watanzania.

Matumaini yangu kupitia maonesho haya ni kwamba, Wananchi tumepata uelewa wa utekelezaji wa mambo ya Muungano kwa kutambua fursa zilizopo na hivyo tusisite kuzitumia ipasavyo kwa manufaa yetu na urithi kwa vizazi vijavyo. Amani na utulivu wa Nchi yetu imekuwa ni chachu ya maendeleo yetu kwani Wananchi tuko salama, tukiwa na mshikamano, kuaminiana katika masuala ya kisiasa na kujiendeleza kiuchumi.

Kuinua Uchumi

Ndugu wananchi;

Sote tunadhihirisha kuwa, Muungano huu umesaidia sana kuimarisha hali za Wananchi na kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano. Katika mageuzi ya uchumi yanayoendelea, Serikali imeweka mazingira mazuri kwa Sekta Binafsi ili kuziwezesha kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi. Hivi sasa kuna ongezeko kubwa la mitaji ya moja kwa moja kutoka nje na mitaji ya ndani. Zipo fursa nyingi kwa Wananchi wa pande zote mbili za Muungano kuwekeza katika Sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, kujenga viwanda, hoteli za kitalii na nyumba za biashara za kuishi bila bughudha kutoka pande zote za Muungano. Hali hiyo imechangia katika kuongeza ajira kwa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Aidha, uwepo wa soko la pamoja lisilokuwa na vikwazo vya kiutawala na kiuendeshaji limeweka mazingira ya ushirikiano na kuleta utangamano wa kiuchumi. Hali hii imesababisha mtiririko wa rasilimali na bidhaa, mitaji, watu na huduma baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuimarika na hivyo kukuza biashara kwa kiasi kikubwa na uchumi kwa ujumla. Maonesho haya yanadhihirisha kwamba Muungano wetu umekuwa wa mafanikio makubwa.

Hitimisho

Ndugu Wananchi;

Katika kuhitimisha maonesho haya, tukio hili la maonesho liwajengee mwamko wa kujifunza na kuelewa masuala ya Muungano na utekelezaji wake. Serikali zetu pamoja na taasisi zake zitaendelea kuelimisha umma kupitia njia mbalimbali za kupashana habari, ikiwemo majarida, vipindi vya redio na televisheni, matamasha, na maonesho mengine ya kitaifa. Nawasihi Watanzania wenzangu tusichoke kutaka kujua masuala mbalimbali yanayohusu Muungano wetu kwa lengo la kuimarisha na kutumia fursa zilizopo. Tuepuke dhamira yoyote ya kutaka kuvunja Muungano.

Serikali kupitia Taasisi zetu zitahakikisha Wananchi wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya Muungano wetu, na kutumia fursa zilizopo kujiendeleza na hatimae kuimarisha Muungano wetu zaidi.

Napenda kutoa wito kwa Viongozi Watendaji na Wananchi kila mmoja katika nafasi yake kukumbuka kuwa, Muungano wetu umedumu kwa miaka 50, hivyo basi, yatupasa **kuulinda, kuuimarisha** na **kuudumisha**. Tupime tulikotoka, tujiangalie tulipo sasa, na tujipange kwa miaka ijayo ili kuwa na Muungano ulio imara na wenye mafanikio zaidi ya haya tuliyoyafikia kwa mustakabali wa taifa letu.

Ndugu Wananchi;

Mwisho, nawatakia Watanzania kheri na mafanikio katika shamrashamra hizi za maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano. Waliopata fursa ya kutembelea maonesho hayo wawe Mabalozi wa kweli wa Muungano wetu kupitia waliyoyashuhudia na kujifunza katika maonesho haya. Tuna kila sababu ya kujivunia kuwa Watanzania na maendeleo tuliyopata kwa miaka 50 kwa kuwa ***Utanzania Wetu ni Muungano Wetu; Tuulinde, Tuuimarishe na Kuudumisha.***

Kwa haya machache napenda sasa kutamka kwamba, **Maonesho haya Maalum ya Miaka 50 ya Muungano yamefungwa rasmi.**

Asanteni kwa kunisikiliza.